# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**

Natumia nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba Mbingu na Ardhi na kila kilichomo ndani yake kwa kutuwezesha kukutana leo katika chombo hiki muhimu cha kutunga sheria tukiwa wazima wa afya kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba ya kuwatumikia wananchi.

**Mheshimiwa Spika**,

kwa niaba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**,

Pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa juhudi kubwa wanazozichukuwa katika kuimarisha sekta ya elimu nchini. Aidha,

napenda kumshukuru Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa maono, ushauri, mawazo na miongozo anayompatia Mheshimiwa Rais, katika kuhakikisha nchi inazidi kupiga hatua katika kujiletea maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Maunzo ya Amali, Mheshimiwa Lela Muhammed Mussa, Naibu Waziri Mheshimiwa Khadija Salum Ali, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada kubwa wanazozichukuwa katika kuipeleka mbele Sekta ya Elimu nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Shukurani za pekee ziwaendee wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa namna walivyoshiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa kupitia bajeti ya Wizara hii. Wajumbe walionesha umahiri na ukomavu wao katika kuijadili na kuichangia na hatimae leo hii kufikishwa mbele ya Baraza lako tukufu ikiwa na lengo la kuisaidia Serikali kutimiza malengo yake kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima kubwa naomba niwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Dkt. Nasra Nassor Omar | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Seif Hamad Suleiman | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Shaame Ali Ali | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Issa Ussi Haji (Gavu) | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Zainab Khamis Shomari | Mjumbe |

8. Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri — Katibu
9. Ndg. Mussa Issa Mussa — Katibu
   Ndg. Mohamed Raymond Mwellu — Afsa Bajeti

**Mheshimiwa Spika,**

Kanuni ya 101(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2024, inaelekeza kwamba, "*Makadirio ya Wizara kwanza yatajadiliwa na Kamati husika kabla ya kujadiliwa na Baraza na hayatapelekwa kwenye Baraza wala Kamati ya Matumizi mpaka Mwenyekiti wa Kamati iliyopewa kazi hiyo atakapomuarifu Spika kwamba Kamati yake imemaliza kuyafikiria Makadirio hayo.*"

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Ustawi wa Jamii imetimiza takwa hili la kikanuni na ilifanikiwa kukaa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na hatimae kupitia na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Ustawi wa Jamii ilikaa na kuipitisha bajeti ya Wizara hii kwa kutoa maelekezo na ushauri katika baadhi ya maeneo ambayo yanaonekana kuwa na changamoto, ambapo Wizara iliahidi kuzifanyia kazi changamoto hizo, ili malengo ya Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka huu wa fedha yaweze kukamilika kwa wakati na kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka 2026/2027, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imepanga kutekeleza Programu kuu tano kama zifuatazo:-

i) Programu Kuu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi;

ii) programu Kuu ya Elimu ya Sekondari;

iii) programu Kuu ya Elimu ya Juu;

iv) programu Kuu ya Elimu Mbadala na Watu Wazima;

v) programu Kuu ya Ubora wa Elimu; na

vi) programu Kuu ya Uongozi na Utawala.

## PROGRAMU YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii inahusu uimarishaji na utoaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi kwa wanafunzi wenye umri kati ya miaka minne hadi kumi na mbili. Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii ilitengewa jumla ya shilingi **250,051,036,000** kwa matumizi ya kawaida na mishahara ya wafanyakazi na hadi kufikia Machi 2026, Programu hii imefanikiwa kuingiziwa kiasi cha Tsh. **123,878,737,229** sawa na asilimia 49.5 ya Makadirio.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kufikia kiwango kizuri cha uandikishaji wa wanafunzi wa Maandalizi kwa asilimia 94.7 ya shabaha ya utekelezaji na asilimia 106.1 kwa wanafunzi wa Msingi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hatua hii ya maendeleo, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kutoa taaluma iliyo sahihi kwa wanafunzi hao huku wakizingatia Mitaala  na Mihutasari ya masomo husika, ili kuwajengea msingi mzuri wa kujifunza  stadi zote  za kusoma, kuandika na kuhesabu.

**Mheshimiwa Spika,**

Msingi mzuri wa kujifunza kwa wanafunzi wetu unajengwa katika ngazi hizi za Maandalizi na Msingi, hivyo ni vyema kwa walimu wenye dhamana hii kutumia mbinu bora na zenye kufaa zitakazowasaidia watoto hawa kujifunza kwa ufanisi. Waswahili wanasema *"Udongo upate ulimaji na Kambare mkunje bado mbichi."*

## PROGRAMU YA ELIMU YA SEKONDARI

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo la Programu hii ni kuimarisha Elimu ya Sekondari. Katika kulitekeleza hili Wizara imelenga kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kujiunga na skuli za Sekondari na kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapongeza hatua za Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kufanikiwa kuimarisha Sekta ya Elimu nchini kwa kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha sita kwa kufikia asilimia 99.8 ya shabaha ya utekelezaji kwa mwaka 2026. Juhudi zilizotumika hadi kufikia hatua hii kubwa ya maendeleo, zinapaswa kuendelezwa ili kuipaisha zaidi Sekta ya Elimu kitaifa na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ni kiungo muhimu sana katika kuwasaidia wanafunzi wanaomaliza masomo yao ya Sekondari na wanaotaka kujiunga na Elimu ya Juu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wa skuli za Sekondari, kunatoa fursa kwa wanafunzi kujiunga na Elimu ya Juu, hivyo ni vyema kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kuwapatia wanafunzi hao mikopo, ili waweze kuendelea na masomo yao bila ya usumbufu, kama tunavyofahamu kwamba, wazazi wa wanafunzi walio wengi ni wenye kipato cha chini ambao wanashindwa kuwasomesha watoto wao katika ngazi za juu za elimu, hivyo ni wajibu wa Bodi hii kuwatendea haki wale wote wanaohitaji na wenye sifa zinazostahiki, kwa kuwapatia mikopo bila ya ubaguzi wowote.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inapongeza juhudi za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kwa kushirikiana na Taasisi nyengine za Serikali ikiwemo ZSSF kwa ajili ya kuwabaini wanafunzi waliokopeshwa ambao bado hawajarejesha madeni yao. Kamati inaishauri Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kuwafuatilia kwa karibu wale wote ambao waliopewa mikopo na bado hawajarejesha kwa muda mrefu sasa, ili waweze kufaidika na wengine wanaohitaji.

**PROGRAMU YA ELIMU YA JUU**

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo hasa la Programu hii ni kutoa Elimu itakayomuwezesha muhitimu kujiajiri au kuajiriwa, ambapo ndani yake kuna Programu Ndogo ya Mafunzo ya Ualimu ambayo inalenga kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilifanya ziara katika Chuo kipya cha Ualimu Nkurumah na kubaini changamoto kadhaa ambazo zinakwamisha mustakbali na muelekeo wa mafanikio wa wakufunzi waliopo katika chuo hicho kwa sasa. Wakufunzi hao hadi sasa wanalipwa mishahara kama walimu wa Sekondari.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba, Utumishi na Utawala Bora kuliangalia suala la maslahi ya wakufunzi wa Chuo kipya cha Ualimu Nkurumah, ili waweze kufanana na wakufunzi wa vyuo vyengine nchini, hii itasaidia kuwajengea ari na mori wa kutekeleza majukumu yao na kinyume chake ni kuwavunja moyo na kuishushia hadhi Sekta ya Elimu nchini. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwatambua rasmin wakufunzi hawa kama ni wakufunzi wa Chuo kwa kuwapatia stakabadhi sahihi inayoonesha kuteuliwa kwao kuwa wakufunzi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mnasaba huu Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuiingiza fedha yote ilivyokadiriwa kwa Programu hii kwa wakati, ili kuisogeza mbele sekta hii ya Elimu ya Juu nchini. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi **220,223,295,000** fedha ambayo imeongezeka ukilinganisha na fedha iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambayo ni shilingi **84,810,923,000**.

## PROGRAMU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Jumla ya shilingi **120,762,856,000** zimekadiriwa kutumika kwa Programu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, fedha ambayo imeongezeka sana kulinganisha na fedha iliyokadiriwa kwa mwaka 2025/2026 ambayo ni shilingi **11,916,476, 000.**

**Mheshmiwa Spika**,

Programu hii inalenga kuwajengea uwezo vijana ili waweze kukabiliana na soko la ajira, kwa kuwapatia mafunzo ya amali na Elimu Mbadala. Kwa mnasaba huu, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuviimarisha vyuo vya Amali viliopo nchini kwa kuimarisha miundombinu ya majengo, vifaa pamoja na rasilimali watu, lengo hasa ni kuikuza tasnia hii ya Amali na Ufundi kwa vijana wetu. Kamati inapongeza ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya Amali kutoka wanafunzi 2,644 mwaka 2025 hadi kufikia wanafunzi 3,717 mwaka 2026, hii inatoa taswira nzuri kwa vijana kuweza kujipatia ujuzi utakaowawezesha kujiajiri wao wenyewe.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa mara nyengine, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Pia, nawashukuru wajumbe wako wote kwa kutenga muda wao na kunisikiliza kwa makini wakati nikiwasilisha Maoni haya. Nawaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu kuichangia na kuipitisha bajeti hii ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri aweze kutekeleza majukumu aliyojipangia kwa wakati na kwa ufanisi. Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Kamati yangu naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Ahsante sana,

……………………….,

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu,

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**